# TABIA YA MUNGU

Tabia ya Mungu imegawanyika katika pande kuu mbili; ya wema na ukali. Warumi 11:22 maandiko yanasema **"Tazama, basi, wema na ukali wa Mungu, kwa wale walioanguka ,ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, ukikaa katika wema huo; kama sivyo, wewe nawe utakataliwa mbali."**

## I .WEMA:

Huu ni upande wa kwanza wa tabia ya Mungu :hunaonesha wema wa Mungu kwa viumbe vyake. Kutoka 34:6-7 **"BWANA akapita mbele yake, akatangaza, BWANA,BWANA,Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne".**

Yeremia 9:23-24 Mungu anasema **"BWANA anasema hivi, mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi na kunijua, ya kuwa mimi ni BWANA, nitendaye wema na hukumu na haki; katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema BWANA."**

Mtume Yohana pia anatudhibitishia upendo wa Mungu kwa jamii ya wanadamu . Katika 1Yohana 4:16,19. **"Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake. Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza."**

## II.UKALI:

Huu ni upande wa pili wa tabia ya Mungu. Ili aitwe Mungu mwenye haki ni pale anapompa mkosaji haki yake na mwema haki yake. Jambo hili amelisema mwenyewe katika sheria aliyoitamka pale Sinai kutoka 20:5-7 "usivisujudie wala kuvitumikia, kwa kuwa mimi, BWANA Mungu wako, ni Mungu wenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu. Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA

**Commented [U1]:** Mungu hana tabia mbili. Kusema hivyo ni kudai kwamba Mungu ana kigeugeu. Tabia yake ni moja: ″Mungu ni upendo.″ Kwa hiyo, chochote tutakachosema kuwa ni tabia yake ni tawi tu la upendo. Hakuna andiko lolote linalosema kwamba Mungu ni wema; bali wema ni tawi la tabia ya Mungu ambaye ni upendo.**

**Hapa basi, suala siyo wema na ukali, bali ni upendo na hayo mawili. Je, tafsiri yako kuhusu mambo hayo mawili yanaambatana na upendo? Tatizo hapa si kukusanya mafungu, bali je, tafsiri yako ya hayo mafungu inalingana na tabia ya Mungu ambaye ni upendo?**

**Upendo si sawa na wema, bali wema ni sifa ya upendo.**

--

**Commented [U2]:**
Kwa muhtasari, kinacholengwa hapa ni kudai kwamba Mungu hutenda mema na mabaya. Yaani, Mingu anapotenda wema basi mtu hupokea mema, na anapotenda kwa ukali basi mtu hupokea mabaya.
Hii ndiyo maana ya kusema Mungu ana sehemu mbili. Huyu Mungu yuko nyuma ya ule mti wa mema na mabaya – Mwanzo 2:17.
Mungu yupi aliye na sura mbili? Ni yule aliyewakilishwa na huu mti.

Katika maandiko, Mungu ameelezwa kuwa chemchemi ya uzima. Soma (Zaburi 36:9; Mithali 13:14; Mithali 14:27). Kwa hiyo, mti wa uzima unamwakilisha Mungu na tabia yake.

Inabaki basi kwamba ule mti mwingine ulimwakilisha Shetani. Kutoka kwake tunapata vipande vidogo vya udanganyifu vilivyofunikwa kwa wema fulani lakini vikiwa na sumu na nia ya uovu.

"Shetani, akiwa amejifunika kwa udanganyifu, bado anajificha katika mti wa maarifa ya wema na mabaya." – {GCDB, Machi 6, 1899, kifungu cha 4} ...

**Commented [U3]:** Msisitizo hapo ni kwamba Mungu ndiye apeane. Basi Ukisema Kinyume na hilo , unaitwa mwasi. Hii hoja ni kweli ? Wanaodai hili wao wenye wataisimamia hadi mwisho tukianza kuipima ? ?

Hebu tujaribu.
Ukila vibaya, ukawa muhanga wa ulafi wa nyama ukapata saratani ya utumbo mwembamba, Mungu ndiye amekupa huo ugonjwa? Nani akakupa adhabu hiyo?

Ukiwa mraibu wa sigara, hadi ukapata mangojwa, nani kukuadhibu?

Je, hauoni kwa hoja hiyo, inafaa Mungu awe ndiye wakupeana virusi vya ukimwi kwa mzee anayefanya husherati Kariako? Tena huyo Mzee aliyeoewa virusi hivyo na Mungu akapeleka nyumbani kwa mke wake aliyemwaminfu kwa huyo huyo Mungu?
Labda tusongebele kidogo kwa ibada.
Ukiabudu Miungu mingene na kutafuta wenye pepo, hadi ...

hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajae jina lake bure." Pia katika kutoka 34:7 inasema **" ----wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe----"** kauli hizo huonesha jinsi ambavyo Mungu anavyoshughulika na waovu na wavunjaji wa sheria na maagizo yake. Baada ya hatua zote za kuwasihi warudi na kuacha maovu yao kushindikana, hutoa adhabu.

Katika upande huu wa pili wa tabia ya Mungu, kuna udhibitisho mwingi sana wa maandiko yakionesha Mungu akitoa idhini waovu kuadhibiwa na kuangamizwa kutokana na maovu waliyotenda. Kuna wakati aliwaagiza wanadamu na Malaika kutekeleza mauaji kwa waasi, lakini pia kuna wakati anaonekana Mungu mwenyewe akitekeleza jukumu la kuwaangamiza waovu.

## A: KUWATUMIA WANADAMU

1Samweli 15:2-3 **"Bwana wa majeshi anasema hivi, Nimeyatia moyoni mwangu mambo hayo Amaleki waliyowatenda Israel, jinsi walivyo wapinga njiani, hapo walipopanda kutoka Misri. Basi sasa enda ukawapige Amaleki, na kuviharibu kabisa vitu vyote walivyo navyo, wala msiwaachie; bali waueni, mwanaume na mwanamke, mtoto naye anyonyaye, ng'ombe na kondoo, ngamia na punda."** Huyo ni mfalme Sauli akipewa maagizo hayo na Bwana kupitia kinywa cha Nabii Samweli.

Katika Ezekieli 9:5-6 **"Na hao wengine aliwaambia, nami nalisikia, piteni kati ya mji nyuma yake, mkapige; jicho lenu lisiachilie, wala msione huruma. Waueni kabisa, mzee na kijana, na msichana na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu yeyote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika patakatifu pangu. Basi wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba."** Hapo ni wakati Mungu anawaagiza watu sita aliowaita na kuwagiza kuwaangamiza wakazi wa Yerusalemi waliokuwa wamemuasi na kukataa maonyo. Nabii Ezekieli anasikia maagizo hayo yakitolewa na Mungu mwenyewe.

## B. KUWATUMIA MALAIKA

Isaya 37:36 **"Basi Malaika wa BWANA alitoka, akaua watu mia na themanini na tano elfu katika kituo cha waashuri, na watu walipoamka asubuhi na mapema, kumbe, hao walikuwa maiti wote pia."** Huu ni wakati mfalme wa Ashuru, yaani Senakeribu alipojitapa kuangamiza Yuda, mfalme Hezekia akamlilia

**Commented [U4]:**
Ni jambo la kawaida kuelewa kwamba Mungu hatakuhesabu bila hatia ikiwa utakuwa mkaidi katika dhambi zako. Hata hivyo, hilo si sawa na kusema kwamba kile kitakachokupata kwa sababu ya dhambi zako kimetoka kwa Bwana.

Sauli alikuwa amemkataa Mungu, na Mungu akamtuma nabii kumwambia kwamba Mungu amemkataa. Lakini unawezaje kumkataa mtu ambaye tayari amekukataa? (1 Samweli 15:23). Lugha hiyo inaeleweka tu tukitambua kwamba Mungu aliheshimu uamuzi wa Sauli wa kumkataa Mungu.

**Commented [U5]:**
Kanuni inayozungumziwa hapa ambayo bado haijaeleweka vizuri ni kwamba Mungu ametumia na ataendelea kutumia dhambi kuadhibu dhambi.

"...kuadhibu dhambi kwa dhambi." {PP 728.1}

...

**Commented [U6]:** Ikiwa hujaelewa mfano huo , basi huu mwingene utasaidi.

Yohana 13:27 - Yuda alipokwisha pokea kipande hicho, Shetani akamwingia. Basi Yesu akamwambia, "Unachotaka kufanya, kifanye haraka!"

...

**Commented [U7]:**
2 Samweli 14:47
Hivyo Sauli akautwaa ufalme juu ya Israeli, akapigana na adui zake wote pande zote, dhidi ya Moabu, na dhidi ya wana wa Amoni, na dhidi ya Edomu, na dhidi ya wafalme

...

**Commented [U8]:** Kazi hii ni sawa na ile ya Malaika wa ufunuo 7.

**Commented [U9]:** Je, hili limeandikwa kwa ajili ya kunukuu tu? Au mwandishi anamaanisha kwamba baadaye kulikuwa na watu sita waliopita Yerusalemu na kuua watu hekaluni na mjini?

...

**Commented [U10]:** Malaika hutumwa kutoka korti za mbinguni, si kwa **ajili ya kuharibu,** bali kwa ajili ya kuwalinda na kuwatunza nafsi zilizo hatarini, kuwaokoa waliopotea, na kuwarudisha waliotangatanga katika zizi. " Sikuja kuhukumu, bali kuokoa," Kristo alitangaza.

...

**Commented [U11]:** Kamwe malaika wanaposhuka "Walishuka kwa nguvu kuu, si kwa ajili ya kuua, **wala si kwa ajili ya kudai heshima**, bali kwa ajili ya kupiga kambi kuzunguka na kuhudumia wale wa Bwana waliokuwa dhaifu na wasio na msaada."

...

**Commented [U12]:** Neno hilo hilo ambalo huku Kiswahili imetafsiri kuua linasoma hivi .

2 Samweli 24:10
Ndipo moyo wake Daudi UKAMCHOMA baada ya kuwahesabu hao watu. Naye Daudi akamwambia BWANA

...

Mungu, ndipo Mungu alipomtuma Malaika wake kuwaua wanajeshi wa jeshi la Senakeribu.

Pia katika maangamizo ya wazaliwa wa kwanza wa wamisri na wa wanyama wao, Mungu alimuagiza Malaika kutekeleza mauaji hayo. Kutoka 12:29 **"Hata ikawa, usiku wa manane BWANA akawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, tangu mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi katika kiti chake cha enzi, hata mzaliwa wa kwanza wa mtu aliyefungwa katika nyumba ya wafungwa; na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama."** Nabii akielezea utekelezwaji wa tukio hilo anaelezea lilifanywa na Malaika aliyeagizwa kuwaua wazaliwa wote wa wamisri **"Waisraeli walitii maagizo ambayo Mungu aliwapatia -----Akina baba na akina mama waliwashika katika mikono yao wapendwa wao wazaliwa wa kwanza kadri walivyofikiri kuhusu pigo lililokuwa tayari kumwagwa usiku ule. Lakini hakuna makazi ya waisraeli yaliyotembelewa na Malaika muuaji. Ishara ya damu ya ulinzi –ishara ya ulinzi wa mwokozi –ilikuwa katika milango yao, na muharibifu hakuingia."** Ellen G. White Wazee na Manabii 264.2(PP 279.3) Kuhusu maagizo ya Sodoma na Gomora, tunamuona Mungu akiwatumia Malaika kuteketeza tukio hilo, maana Bwana alikuwa amemjulisha rafiki yake Ibrahimu kile wanachoenda kukifanya Sodoma. Fatilia mazungumzo kati ya Bwana na Ibrahimu utatambua kuwa si shetani aliyetekeleza tukio hilo bali ni Bwana kupitia Malaika aliokuwa amewaagiza. Mwanzo 18:22-33 **"Basi wale watu wakatoka huko wakaelekea Sodoma, lakini Ibrahimu alikuwa akali akisimama mbele za BWANA. Ibrahimu akakaribia, akasema, je, utaharibu wenye haki pamoja na mwovu? Huenda wakawapo wenye haki hamsini katika mji,utaharibu, wala hutauacha mji kwa ajili ya hao hamsini wenye haki hamsini waliomo? Hasha usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hasha, mhukumu ulimwengu wote asitende haki? BWANA akasema, nikiona katika Sodoma wenye haki hamsini mjini nitapaacha mahali pote kwa ajili yao. Ibrahimu akajibu akasema, basi, nimeshika kusema na Bwana, nami ni mavumbi na majivu tu. Huenda wakapunguka watano katika wale hamsini wenye haki, je utaharibu mji wote kwa kupungua watano? Akasema, sitauharibu, nikiona humo arobaini na watano. Akazidi tena kusema naye akinena, huenda wakaonekana humo arobaini? Akasema sitafanya kwa ajili hao arobaini. Akasema, Bwana asiwe na hasira,**

**Commented [U13]:** Neno katika kiingeleza sio " akaua ' bali akawapiga. Hii hapa KJV

37:36 Then the angel of the LORD went forth, and SMOTE in the camp of the Assyrians a hundred and fourscore and five thousand: and when they arose early in the morning, behold, they [were] all dead corpses.

**Commented [U14]:** Sasa malaika alichokifanya ni kuwapiga, na wala si kuwaangamiza. Lakini, malaika aliwapiga wapi? Kwa kutumia fimbo ipi?

Malaika wa Mungu hutumwa kwa neno (Waebrania 1:7). Neno hupiga mawazo au moyo. Vita vya damu na nyama ni vya kibinadamu. Angalia hapa:

Neno hilo hilo limetumika wakati Daudi alihesabu Waisraeli (2 Samweli 24:10).

**Commented [U15]:** Sasa tuunganishe fungu hilo na haya mengine.

kutoka 12:23. Maana mimi Mwenyezi-Mungu nitapita kuwaua Wamisri. Lakini nitakapoiona damu iliyopakwa kwenye vizingiti na miimo ya nyumba zenu, nitazipita na wala **sitamruhusu mwangamizi** kuingia katika nyumba zenu na kuwaua.

Zaburi 78:49

"Aliwatumia joto la ghadhabu yake, chuki yake kali, akawaachilia malaika waovu kati yao." ( BBE)

Nani ni Mwangamizi?

1 Wakorintho 10:10

"Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyofanya, wakaangamizwa na Mwangamizi."

Ufunuo 9:11 ...

**Commented [U16]:** Ninashangaa tena, je, nukuu hii imeeleweka? Inawezekanaje mtu kuitumia kuthibitisha kwamba malaika wa Mungu huua? Ni nani malaika aliye muuaji? (Yohana 8:44, Yohana ...)

**Commented [U17]:**
Ni nani tena Mwangamizi?

Katika Maandiko anaitwa Mwangamizi, mshtaki wa ndugu, mdanganyifu, mwongo, mwenye kutesa, na muuaji. Shetani ana wengi wanaomfanyia kazi, lakini hufanikiwa zaidi anapoweza kutumia Wakristo wa kujidai kwa kazi yake ya kishetani.
— {5T 137.4}

**nami nitasema, huenda wakaonekana huko thelathini? Akasema sitafanya nikiona humo thelathini. Akasema, tazama nimeshika kusema na Bwana, huenda wakaonekana huko ishirini? Akasema, sitaharibu kwa ajili ya hao ishirini. Akasema, Bwana asiwe na hasira, nami nitasema mara hii tu, huenda wakaonekana huko kumi? Akasema sitaharibu kwa ajili ya hao kumi. Basi Bwana alipokwisha kuzungumza na Ibrahimu akaenda zake; Ibrahimu naye akarudi mahali pake.”**

Nabii akielezea jinsi maangamizi ya Sodomo yalivyofanywa, na waliohusika kuyatekeleza, anasema **“Kisha Malaika wakawaacha na kurudi Sodoma ili kukamilisha kazi yao ya maangamizi. Mwingine –ambaye Ibrahimu alimsihi, alikuja karibu na Lutu. Katika miji yote ya bondeni hapakuwepo na wenye haki hata kumi; lakini wakijibu ombi la mzee, mtu ambaye alimcha Mungu alitolewa ili asiangamizwe. Amri ilitolewa kwa hisia kali, “Jiponye nafsi yako usitazame nyuma wala usisimame katika hilo bonde wala popote, ujiponye mlimani, usije ukaangamia … ” Ellen G. White, Wazee na Manabii uk 140.1(PP 160.2).** Hapo tunaona ni Malaika wa Bwana ndio waliorudi Sodoma kuangamiza miji hiyo ya Bondeni baada ya kumtoa Lutu na familia yake.

Pia Nabii Isaya alitabili angamizo la Babeli litakuwa kama jinsi Mungu alivyoangamiza miji ya Sodoma na Gomora. **“Tazama, nitawaamsha Wamedi juu yao, hawaoni fedha kuwa kitu, wala hawafurahii dhahabu. nyuta zao zitawangusha vijana; wala hawatahurumia mazao ya tumbo; jicho lao halitawahurumia watoto. Na Babeli, huo utukufu wa falme, uzuri wa kiburi cha Wakaldayo, utakuwa kama Sodoma na Gomora hapo Mungu alipoiangamiza”** Isaya 13:17-19

## C.MUNGU MWENYEWE

Hapa kuna uthibitisho wa kuonesha Mungu akitoa hukumu kwa waovu baada ya kukataa rehema zake, pia ndiye mwenye kuwarudisha watu mavumbini pale asemapo rudi. Ana uwezo wa kuondoa uhai na kuurejesha.

Katika 1Samweli 2:6 tunasoma **“BWANA huua, naye hufanya kuwa hai; hushusha hata kuzimu, tena huleta juu.”** Mtunga zaburi anasema “**Wewe Bwana umekuwa makao yetu, kizazi baada ya kizazi. Kabla haijazaliwa**

**Commented [U18]:** Je, unaweza kuonyesha kutoka katika vifungu vile viwili vilivyonukuliwa mahali uliposoma kwamba malaika walipokuwa Sodoma walikwenda kuharibu na kuchoma watu?

Kwanza, yule aliyebaki kuzungumza na Abrahamu alikuwa Kristo, si malaika.
Pili, wale malaika waliotangulia kwenda Sodoma, kazi iliyorekodiwa kwetu kwamba walifanya ilikuwa kumwokoa Lutu.

**Commented [U19]: Nilionyeshwa kwamba hukumu za Mungu hazitoki moja kwa moja kutoka kwa Bwana juu yao, bali kwa njia hii:** Wao hujiweka wenyewe nje ya ulinzi Wake. Yeye huonya, hurekebisha, husema kwa ukali, na huonyesha njia ya pekee ya usalama; kisha ikiwa wale waliokuwa wakipokea uangalizi Wake wa pekee watafuata njia yao wenyewe bila kujali Roho wa Mungu, baada ya maonyo ya mara kwa mara, wakichagua njia yao wenyewe, basi Yeye hamwamuru malaika Wake kuzuia mashambulizi makali ya Shetani juu yao.

— 14MR 3.1

**milima, wala hujaiumba dunia, na tangu milele hata milele ndiwe Mungu. Wamrudisha mtu mavumbini, usemapo rudini, enyi wanadamu."** Zaburi 90:1-3 "**Wewe wauficha uso wako, wao wanafadhaika, waiondoa pumzi yao, wanakufa, na kuyarudia mavumbi yao."** zaburi 104:29

Tunashuhudia pia wakati wa wana wa Israel walipolilia nyama, Mungu alichukizwa, na hasira yake ikawaka juu yao, akawaua wengi kutokana na tamaa yao. Hesabu 11:33-34 **"Kisha hapo hiyo nyama ilipokuwa ikali kati ya meno yao, hawajaitafuna bado, hasira za BWANA ziliwaka juu ya watu, BWANA akawapiga watu kwa pigo kuu mno. Jina la mahali pale likaitwa kibroth-hataava; maana ni hapo walipowazika hao watu waliotamani"** Mtunga Zaburi akielezea tukio hilo hilo anasema: **"hawakuachana na matakwa yao. Ila chakula chao kikali ki vinywani mwao, hasira ya Mungu ikapanda juu yao, Akawauwa waliokuwa wanono**"zaburi 78:30-31

Nabii Nahumu akimweleza Mungu jinsi alivyo kuhusu upande huu wa pili wa tabia yake ya ukali anasema **"Bwana ni Mungu mwenye wivu, naye hujilipiza kisasi; Bwana hujilipiza kisasi juu ya adui zake, huwawekea adui zake akiba ya hasira. Bwana si mwepesi wa hasira ana uweza mwingi, wala hatamhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; BWANA ana njia yake katika kisulisuli na tufani, na mawingu ni mavumbi ya miguu yake. Yeye huikemea bahari na kuikausha, pia huikausha mito yote; Bashani hulegea,na Karmeli; Bashani hulegea , na karmeli ; hulegea nalo ua la Lebanoni. Milima hutetemeka mbele zake, navyo vilima huyeyuka; nayo dunia huinuliwa mbele za uso wake, naam, dunia na wote wakaao ndani yake. Ni nani awezaye kusimama mbele za ghadhabu yake, naye ni nani awezaye kukaa katika ukali wa hasira yake? Hasira yake kali humwagwa kama moto, nayo majabali ya pasuliwa na yeye."** Nahumu 1:2-6. Huyu ndiye Mungu yule mwenye huruma na upendo ila akikasilika dunia yote hutetemeka mbele ya utisho wake.

Mungu alimuuliza Ayubu swali, juu ya silaha zake za maangamizi atakazozitumia siku ya vita dhidi ya waovu **"Je? umeziingia ghala za theluji, Au umeziona ghala za mvua ya mawe, nilizoziweka akiba wakati wa misiba, kwa siku ya mapigano na vita?"** Ayubu 38:22-23

Mtume Petro naye anatujulisha kuwa dunia hii Mungu ameiweka akiba kwa ajili ya kuichoma moto **"Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa**

**Commented [U20]:** Alafu , ni nini ilioyo waua , ni nyama , au mungu , au joto kali ?

…Mungu aliwapa nyama, kama walivyotamani, naye akawaacha wapate matokeo ya kuridhisha tamaa zao za mwili. Homa kali ziliwaangamiza watu wengi sana… CD 377.3

Wewe hata huna haya kupandikizia Mungu kifo hicho?

**Commented [U21]:**
. Walipewa nyama, na kwa tamaa wakaila hadi wakafa. Unawezaje kumlaumu Mungu kwa tamaa isiyodhibitiwa ya wanadamu?

"Walipendelea utumwa, na hata kifo, kuliko kunyimwa nyama. Mungu, kwa hasira yake, aliwapa nyama ili kuridhisha tamaa zao za mwili, na idadi kubwa yao walikufa walipokuwa wakila ile nyama waliyoitamani."

— {RH, Juni 6, 1899, aya ya 7}

Uhalifu na magonjwa yameongezeka katika kila kizazi kinachofuata. Kutokua na kiasi katika kula na kunywa, na kujitumbukiza katika tamaa za chini, kumezizima uwezo wa juu wa akili. Tamaa, kwa kiwango cha kutisha, imekuwa ikidhibiti akili.

— {RH, Juni 6, 1899, aya ya 8}

Mfano: Hii ni kama wanaume ambao Mungu amewaruhusu kuoa kwa sababu ya tamaa zao, kisha wakatumia dawa za kuongeza nguvu za mwili na kufa kwa sababu hawataki kujitenga na tamaa za mwili wao. Je, hilo ni kosa la Mungu?

Hapa Biblia inapotaja kwamba "aliwaua waliokuwa wanene" ni kama kusema "alimwua Sauli." Yaani, kile ambacho Mungu hakukizuia, kinasemekana kana kwamba Yeye ndiye alikifanya. Hii ndiyo hoja ya msingi: mara nyingine Biblia husema Mungu alifanya jambo ambalo kimsingi aliwaruhusu au hakuzuia litokee.

**moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu**"2Petro 3:7

Manabii wakielezea tukio la kuangamizwa kwa waovu kupitia mapigo na kuchomwa moto, tukio hilo wamelielezea wazi. **"Na waliouwawa na BWANA siku ile watakuwapo toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili; hawataliliwa, wala kukusanywa, wala kuzikwa; watakuwa samadi juu ya uso wa nchi."**Yeremia 25:33

Nabii wa Patmo anasema**"Kisha nikaona Malaika mmoja amesimama katika jua; akalia kwa sauti kuu, akiwaambia ndege wote warukao katikati ya mbingu, njoni mkutane kwa karamu ya Mungu iliyo kuu; mpate kula nyama ya Wafalme na nyama ya majemedari, na nyama ya watu hodari, na nyama ya farasi na ya watu wote. wawapandao, na nyama ya watu wote waungwana kwa watumwa, wadogo kwa wakubwa. Kisha nikamuona huyo mnyama, na wafalme wa nchi, na majeshi yao wamekutana kufanya vita na yeye aketiye juu ya farasi yule, tena na majeshi yake. Yule mnyama akakamatwa na yule nabii wa uongo pamoja naye, yeye aliyezifanya hizo ishara mbele yake, ambazo kwa hizo aliwadanganya watu wale waliopokea ile chapa ya huyo mnyama, nao walioisujudia sanamu yake; hao wawili wakatupwa wangali hai katika lile ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti; na wale waliosalia waliuwawa kwa upanga wake yeye aliyeketi juu ya yule farasi, upanga utokao katika kinywa chake. Na ndege wote wakashiba kwa nyama zao."** Ufunuo 19:17-21

Nabii Yohana anaonyesha pia maangamizi ya shetani **"Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, shetani atafunguliwa kifungoni mwake; naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa. Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala. Na yule ibilisi mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele."** Ufunuo 20:7-10

Yesu naye alitoa uhakikisho huo wa kumwangamiza shetani na Malaika zake, pamoja na wanadamu waasi kwa njia ya moto utakaotoka mbinguni. **"Kisha**

**akawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, ondokeni kwangu mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayali Ibilisi na malaika zake; Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele"**Mathayo 25:41,46.

Nabii Ellen G White naye anaonyesha jinsi Mungu atakavyowahukumu kwa kuwangamiza wote watakaokataa rehema yake ya muda mrefu ya kuwasihi. **"Uvumilivu ambao Mungu aliuonesha kwa watu waovu, uliowafanya watu wazidi kukua katika uasi; lakini adhabu yao haitakuwa ndogo kwa sababu ya kuchelewa. "Maana BWANA ataondoka kama vile katika mlima Perasimu ataghadhibika kama vile katika bonde la Gibeoni; apate kufanya kazi yake ya ajabu; na kulitimiza tendo lake, la ajabu**" **Isaya 28:21. Kwa Mungu wetu mwenye rehema, kitendo cha adhabu ni kigeni. "Kama mimi niishivyo, asema Bwana, sikufurahi kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya" Ezekieli 33:11. Bwana ni mwingi wa rehema na kweli, mwenye fadhili ---mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi" na bado "sio mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe" Kutoka 34:6-7. Wakati hafurahiii kulipiza kisasi atatoa hukumu kwa waasi wa sheria yake. Analazimishwa kufanya hivyo, ili kuwalinda wakazi duniani dhidi ya kuharibu kwa tabia na maangamizo. Ili kuwakomboa watu, baadhi wa watu lazima awakate wale ambao wamekuwa wagumu katika dhambi. "Bwana si mwepesi wa hasira, anauweza mwingi, wala hata mwesabia mtu mwovu kuwa hana hatia" Nahumu 1:3.Kwa mambo makuu ya haki atahithibitisha mamlaka ya sheria yake iliyokanyagwa. Na ukweli kwamba yeye huchelewa kutekeleza haki kuonyesha kwamba dhambi huongezeka zaidi kiasi cha kuita hukumu zake na kutoa hukumu kali anayostahili muasi**" Wazee na Manabii 649.1(PP 628.1)

Nukuu hiyo inatuonyesha kwamba si wakati wa mwisho tu ndipo waovu wataangamizwa na Bwana, lakini hata katika maisha ya kila siku, Mungu huendelea kuwakata (kuwauwa)wanaokithiri katika uovu, kwa kuhatarisha maisha ya watu wema.

Pia Nabii anaendelea kuonesha **"Nimeamriwa kuwa saa ya Bwana ifikapo, ikiwa hakuna mabadiliko yaliyofanyika katika mioyo yenye kiburi na majivuno, na ya wenye kutaka makuuu, watu wataona kuwa mkono ule**

**ambao ulikuwa na nguvu kuokoa utakua wenye nguvu kuangamiza. Hakuna nguvu duniani iwezayo kuzuia mkono wa Mungu. Wala akuna vifaa viwezavyo kutumiwa katika kujenga majengo ambavyo vitayalinda yasiharibiwe saa ya Mungu iliyowekwa ifikapo kuwapatiliza watu uasi wao juu ya sheria yake na kujitakia makuu….**" Nuru Safarini/ 1Kutayarisha Njia sura ya 2uk 46.2

Yesu akizunguza na wanafunzi wake aliwataka watambue yule wanayepaswa kumuogopa zaidi kati ya Mungu au mwanadamu "**Msiwaogope wauwao mwili, wasiwaze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanamu"** Mathayo 10:28

Yesu anatutaka tujue anayeangamiza vyote viwili yaani mwili na roho ni Mungu, Katika jehanamu.

Wengi husema Yesu alipokuja hapa duniani alikuja kuifunua tabia ya Mungu ya wema, upendo, rehema na msamaha; ni kweli kabisa, ila hufumba macho yao kuona pia jinsi Yesu alivyofunua tabia ya Mungu ya ukali, japokuwa hakuua mtu

ila hasira aliyoidhihirisha iliashilia adhabu ya hukumu. Tukio la kudhihirisha tabia ya Mungu ya ukali aliidhihilisha katika tukio la kuwaondoa wafanya biashara hekaluni walipogeuza nyumba ya baba yake kuwa sehemu ya biashara**. "Akaona pale hekaluni watu waliokuwa wakiuza ng'ombe na kondoo na njiwa na wenye kuvunja fedha wameketi. Akafanya kikoto cha kambaa akawatoa wote katika hekalu na kondoo na ng'ombe; akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akazipindua meza zao; akawambia wale waliokuwa wakiuza njiwa, yaondoeni haya; msifanye nyumba ya baba yangu kuwa nyumba ya biashara. Wanafunzi wake wakakumbuka ya kuwa imeandikwa, wivu wa nyumba yako utanila."** Yohana 2:14-17

Wengine hudhani kuwa uzito wa dhambi ambazo watakazozibeba waovu ndiyo utakaowaua, jambo hilo si kweli, ingekuwa hivyo Shetani na Malaika zake wangekuwa wamekwisha kuangamizwa na uzito wa dhambi ambazo wamewasababishia wanadamu kutenda tangu uasi ulipoanza pale Edeni miaka maelfu iliyopita, ila bado wapo hadi sasa. Kitakachowaangamiza shetani, Malaika zake na wanadamu waliomwasi Mungu, ni moto wa jehanamu na si vinginevyo.

## FUNDISHO KUHUSU KUUWA WADUDU.

Baadhi ya watu husema akuna chochote kipaswacho kuuwawa hatakama niwadududu waharibifu au wenye kutudhuru. Karama ya unabii inasema ifuatavyo juu ya jambo hili **"Barua zimekuja kwangu, zikiuliza kuhusu mafundisho ya baadhi ya watu wanaosema kwamba hakuna kitu chenye uhai kinachopaswa kuuwawa, hata wadududu, hata kama wanaoudhi au kufadhaisha kiasi gani. Je, inawezekana kwamba mtu yeyeyote anadai kwamba Mungu amempa ujumbe huu ili awape watu?. Bwana hajawai kumpa mwanadamu yeyote ujumbe wa namna hiyo. Mungu hajamwambia mtu yeyote kuwa ni dhambi kuuwa wadudu wanaoharibu Amani na mapumziko yetu. Katika mafundisho yake yote, Kristo hakutoa ujumbe wa namna hii, na wanafunzi wake wanapaswa kufundisha tu kile alichowahamuru."(1SM 170.3)**

**"Ningewaambia kaka na dada zangu, Endeleeni kuwa karibu na mafundisho yanayopatikana katika Neno la Mungu. Kawieni katika kweli nyingi za maandiko. Hivyo ndivyo mnavyoweza kuwa mmoja katika Kristo. Amna muda wa kujihusisha katika mabishano kuhusu mauwaji ya wadudu. Yesu hajaweka mzigo huu juu yenu. "Makapi ni kitu gani kuliko ngano?" (Yeremia 23:28).Masuala haya yanayozuka ni kama nyasi, miti, na makapi ikilinganishwa na ukweli wa siku hizi za mwisho.wale wanaoacha kweli kuu za Neno za Mungu hilikuzungumzia maneno kama hayo awaubiri injili. Wanashughulika na ujanja usio na maana ambao adui huleta ili kuzigeuza akili kutoka kwenye ukweli unaohusu ustawi wao milele. Hawana neno kutoka kwa Kristo kuthibitisha mawazo yao". "Usitumie muda wako katika majadiliano ya mambo kama hayo. Ikiwa una swali lolote kuhusu kile unachopaswa kufundisha, swali lolote kuhusu masomo unayopaswa kukawia, nenda moja kwa moja kwenye hotuba za Mwalimu Mkuu, na ufuate maagizo yake….(1SM 171.1-2)**

Kauli isemwayo na watu kuwa "MUNGU HAUI" imekusudia kumsaidia shetani katika harakati zake za kuwafanya wanadamu wadumu katika dhambi, na wasiogope chochote kihusucho adhabu na hukumu ya Mungu, wala wasiwe na hofu ya kuchomwa moto siku ya mwisho. Kauli hiyo ikipokelewa na kuungwa mkono, tutashuhudia uasi wa kutisha na kupotea kwa roho ya hofu dhidi ya hukumu.

**Commented [U22]:** Hoja hii imepotovu sana na dhaifu. Huwezi kutumia hili kuhalalisha kuua mwanadamu. HAJA KUU hapa ni kwamba Mungu alimwumba mwanadamu akiwa na **uhuru wa kuchagua**. Mwanadamu ni kiumbe wa maadili HURU. Mwanadamu kuua wadudu si sawa na Mungu kuua mwanadamu. Hiyo ni kulinganisha mwanadamu na wadudu. NA MWANADAMU ALIUMBWA KATIKA MFANO WA MUNGU (Mwanzo 1:26).

Kumlinganisha mwanadamu aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu na wadudu ni kumfanya Mungu mwenyewe kuwa kama mdudu.

**Commented [U23]:**

Kwa hoja hii, ni huzuni kwamba watu wanamwabudu Mungu kwa sababu ya hofu ya kuuawa, na si kwa sababu wanaona ubaya wa dhambi.

Ibada ya namna hii ni ya ubinafsi. Hii ndiyo hali halisi ya hofu: hofu huzaa ubinafsi. Ndiyo maana mara nyingi tunataka kwenda mbinguni kwa sababu ya ubinafsi wetu—kutaka kukaa katika nyumba za dhahabu—badala ya kwa sababu tunampenda Mungu.

Lakini upendo hufukuza hofu. Palipo na upendo wa Mungu, tutachukia dhambi kwa sababu ni dhambi. Tutaogopa dhambi si kwa sababu Mungu ni tishio, bali kwa sababu dhambi ndiyo inayotutenga na Baba anayetupenda.

Hii inafanya wokovu kuonekana kama kuepuka mabaya ambayo Mungu atawafanyia wale watakaomkataa. Lakini huo ni utumiaji wa nguvu—ni kama mwanaume anayetoa vitisho ili kupata mke.

**Commented [U24]:** Nguvu ya udanganyifu ya Shetani ilipaswa kuvunjwa. Hii haingeweza kufanywa kwa nguvu. Matumizi ya nguvu ni kinyume na kanuni za serikali ya Mungu; Yeye hutaka tu huduma ya upendo; na upendo hauwezi kuamriwa; hauwezi kushindwa kwa nguvu au mamlaka. Ni kwa upendo tu ndipo upendo huamshwa. — {DA 22.1}

Shetani atafurahishwa sana na kupata ushindi, kwa kuwa na jeshi la waovu wengi watakaochomwa moto pamoja naye katika ziwa la moto kama tulivyoona ushahidi wa maandiko.

Wito wa Mungu kwa wanadamu wote wakati mlango wa rehema haujafungwa: **"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema**"Mithali 28:13

**MUNGU ATUSAIDIE KUJUA UKWELI**

**MAWASILIANO :0768071736**